

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA KIBABII

**(CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHA MASINDE MULIRO)**

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

KIS 200: THEORY AND ANALYSIS OF KISWAHILI LITERATURE

(NADHARIA NA UHAKIKI WA FASIHI YA KISWAHILI)

UTANGULIZI

Kozi hii inalenga kumtanguliza mwanafunzi kuhusu nadharia za uhakiki wa fasihi na jinsi ya kuzitumia nadharia hizo kuhakiki matini mbalimbali za kifasihi. Kozi ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu nadharia za fasihi. Nayo sehemu ya pili inaonyesha jinsi ya kutumia nadharia mbalimbali kuhaki kazi za kisanaa.

MADHUMUNI YA KOZI

Kuchunguza maana ya nadharia za uhakiki na kubainisha namna za kuunda nadharia

Kufafanua namna fasihi inavyoingiliana na jamii

Kuchunguza baadhi ya nadharia na mihimili yake.

Kuchanagana umbo na maudhui katika kazi za sanaa kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia zilizoshughulikiwa darasani.

MATOKEO YA UJIFUNZAJI.

Inatarajiwa kuwa, baada ya kozi hii mwanafunzi ataweza kutekeleza mambo yafuatayo:

Kueleza maana na hatua za kuunda nadharia

Kuchambua kazi mbalimbali za fasihi kwa kutumia nadharia tofauti.

YALIYOMO

Nadharia za uhakiki wa fasihi- Maana, sababu ya kuzizungumzia, Aina za uhakiki, hatua za kuunda nadharia, nadharia mwafaka.

Nadharia za kirasimi: Urasimi wa kimagharibi, Urasimi wa Kiswahili, Urasmi mpya wa Kimagharibi, Urasmi mpya wa Kiswahili.

Ulimbwende

Nadharia za kihalisia: Ki-marx, Uhalisia, Uhalisia wa kijamaa

Udhanaishi

Umuundo

Ufeministi, Usemezano, Udenguzi

Tanbihi: Maana ya fasihi, chanzo, tanzu, fani na maudhui yatashughulikiwa kama sehemu ya uchambuzi. Nadharia nyinginezo pia zitashughulikiwa darasani bali na zile zilizo rodheshwa. Katika nadharia tutashughulikia chanzo na mihimili kama sehemu muhimu ya kozi hii.

UFUNDISHAJI / UTATHMINI WA KOZI

Mwanafunzi atawajibika kuhudhuria mihadhara yote. Mbali na mahudhurio ya mihadhara, atafanya mijarabu miwili ambayo itachangia asilimia thelathini ya jumla ya tuzo katika muhula. Mwishowe mwanafunzi atafanya mtihani ambao utachangia asilimia sabini ya alama za muhula. Mihadhara itaendelezwa kwenye utangulizi. Sehemu kubwa ya somo itaendelezwa kupitia katika mijadala.

Vitabu teule vitakavyosomwa darasani na kutahiniwa

Mfalme Edipode-S. S. Mushi

Kilio cha Haki-A. Mazrui

Rosa Mistika –E. Kezilahabi

Mama Ee-A.K. Mwachofi

Utengano-S. A. Mohamed

Maisha yangu na baada ya miaka Hamsini-S. Robert

Utendi wa mwana Kupona- Kitula, K.

Damu nyeusi-Walibora K. & Mohamed, S.

MAREJELEO

Craig, D. (1975). *Marxists on Literature*. Harmondsworth: Penguin

McDougal, L. (2000). *The Language of Literature*. USA: McDougal Little. Inc.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthilia, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: E. A. E. P

Msolole, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: E. A. E. P

Njogu, K. na chimerah R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Wamitilla, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitilla, K. W. (2002). *Kamusi ya fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Focus Publication

Wamitilla, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi*. Nairobi: Focus Publication Limited

Tanbihi: Marejeleo zaidi yatatolewa darasani.

Mhadhiri: Bi. Muindu K. Gladys – 0721895156